MASHITAKA YA KIMATAIFA DHIDI YA JIANG ZEMIN, RAIS WA ZAMANI WA CHINA

Rais wa Zamani wa China anashutumiwa na wanamazoezi wa Falun Dafa kutoka nchi kumi na mbili duniani kwa tuhuma za mateso na mauaji ya halaiki ("Jinosaidi") kwa binadamu, nchi zenyewe ni: Germany, Taiwan, Spain, Moldova, Armenia, Finland, Iceland, Australia, Belgium, Switzerland, France na Marekani. Maelezo zaidi yanapatikana katika mtandao:
www.flgjustice.org

Charles Lee

Utawala wa serikali ya China umemshikilia Charles Lee, raia wa marekani kwa tuhuma za mazoezi ya Falun Gong. Ameteswa na kupokonywa haki zake kwa kesi halali na ombi lake la kumuona mkuu wa baraza akanyimwa. Kumsaidia ili aachiliwe tembelea mtandao:
www.rescuecharles.org

Jifunze Namna Ya Kufanya Mazoezi
1-877-FALUN-99 www.falundafa.org

Habari Kuhusu Udhalimu
1-888-842-4797 www.faluninfo.net
1-866-FG-FRIEND www.fofg.org

FALUN DAFA NI NINI?

Falun Dafa pia ikijulikana kama Falun Gong ina asili ya mila na desturi za kichina ambayo huboresha binadamu kiakili na kimwili kupitia mtililiko wa mazoezi na kuendeleza "moyo/akili asilia" (Xinxing). Mazoezi haya yamejengwa katika misingi ya **Uaminifu, Kuthamini** na **Uvumilivu**.

Hii desturi ya kale kwa siku za nyuma ilifundishwa faragha na kwa mara ya kwanza ili ilitolewa hadharani mwaka 1992 huko China na Bw. Li Hongzhi. Tangu wakati huo mamilioni ya washiriki duniani kote wamekaririwa wakirpoti kuwa imewaboresha afya na kuimarisha uwezo wao wa kiroho.

MAZOEZI MATANO YA FALUN GONG

Mazoezi tano za Falun Gong yanasaidia kufungua njia za nguvu za mtu kwa haraka; huwezesha uzungukaji wa nguvu mwili mzima; husafisha mwili; hunganisha akili zake, mwili na roho; hupunguza uchovu (stress) na wasiwasi na hufanikisha upatikanaji wa uwezo na amani ya ndani yake. Mazoezi ni rahisi, yenye uwezo mkubwa, rahisi kujifunza na yanaweza kufanywa na watu wa rika zote na wenye afya yoyote ile. Aidha mazoezi haya ni rahisi kuzingatiwa na hata watu wenye shughuli nyingi katika maisha ya kisasa. Hakuna masharti ya ratiba, muda au kituo cha mazoezi. Mtu anaweza kufanya mwenyewe au katika kundi wakati wowote na popote.

Falun Gong
(Falun Dafa)

Mazoezi binafsi ya kujenga akili, mwili na roho

真 善 忍

UAMINIFU KUTHAMINI UVUMILIVU

Zaida ya watu million mia moja wanafanya haya mazoezi ulimwenguni

- Inafaa watu wa rika zote
- Inaondoa uchovu na wasiwasi
- Inaongeza nguvu na maisha marefu
- Inaimarisha afya njema
- Ukuaji mzuri wa kiroho

Shughuli Zote Ni Bure

Hakuna shirika wala haja ya kuwa mwanachama bali kila mtu anaweza kuwa mwanafunzi .

MAFUNZO YA FALUN DAFA

Kitabu kitwaacho **Zhuan Falun** (Uzungukaji wa Gurudumu la Sheria) cha Bw. Li Hongzhi kinatoa mwongozo mzuri na ni kazi muhimu ya Falun Dafa.

Falun Gong ni kitabu cha mafunzo ya awali kwa wonaoanza.

Vitabu vyote viwili vinapatikana kwenye mtandao wa: www.falundafa.org
Pia vinaweza kununuliwa katika duka la vitabu la *Yih Chyun Corp.*
(Simu: 1-888-353-2288 Fax: 1-888-214-2172, http://www.yc-corp.com).

"*Nimekuwa nikifundisha Tai-Chi na kujisomea mambo mbali mbali ya Qigong na mazoezi yake kwa zaidi ya miaka 40, ndipo nilipoanza kufuatilia Falun Dafa. Sasa ninahimiza wanafuzi wangu wafanye mazoezi ya Falun Dafa."-- Haya ni maneno ya Bw. Da Liu ambaye ana umri wa miaka tisini na tano, yeye ni mwalimu wa Tai-Chi huko New York Marekani na mwandishi wa vitabu vinavyohusu afya na kurefusha maisha.*

"Mara nyingi nimejisoma vitabu vya stadi z malezi ya watotoi. Mawaidha yake yalinisaidia kwa muda tu kwani nilikuwa narudia tabia zangu za zamani. Masomo ya Falun Gong yamenifanya kuwa mlezi na mazazi borai na kuongeza nguvu ya maisha yangu." --Hayo ni maneno ya Maureen Zebian (Mwalimu wa shule ya sekondari).

"Falun Gong ni njia ya ajabu ya kumotisha watu binafsi kuwajibika kwa afya yao" -- Dr. Jingduan Yang, MD.

FALUN DAFA NJE YA CHINA

Mazoezi ya Falun Dafa yanafanywa bila usumbufu katika nchi zaidi ya hamsini duniani, kuanzia New York hadi New Delhi na kutoka Geneva hadi Moscow. Vituo vya mazoezi vinandaliwa na kushugulikiwa na wanajamii wa kujitolea. Hakuna malipo wala muundo au uanachama unaohitajika. Kila mtu ni mwanafunzi. Falun Dafa na muanziliahi wake wanatambulika and kutunukiwa na serikali ya China (kabla ya mwaka 1999), miji mingi na majimbo yake huko marekani na baadhi ya nchi mbalimbali. Zaidi ya nishani elfu moja zimetolewa duniani. Wanafunzi wa Falun Dafa ulimwenguni wanaendelea na maombi ya amani kusaidia kukomesha udhalimu nchini China.

FALUN DAFA NDANI YA CHINA

Mwishoni mwa miaka ya 90, Falun Dafa ilikuwa maarufu katika jamii ya wachina, kwani watu 70 hadi 100 million walifanya mazoezi. Licha ya utulivu na kutokua na mwelekeo wa kisiasa, umarufu wa Falun Dafa ulifikiriwa kuwa tishio kwa Mkuu wa Chama cha Kikumunist, na hivyo mnamo Julai 1999 Mkuu, Jiang Zemin aliipiga marufuku. Aidha akaanzisha udhalimu kwa wote wanaofanya Falun Dafa, wengi walifungwa bila hatia, waliteswa na kulazimishwa kazi ngumu. Zaidi ya watu 1000 wamekufa mikononi mwa polisi wa Kichina. Udhalimu umeathiri mamilioni ya watu kwa kupoteza ndugu na jamaa, kazi na haki za msingi.

SOS!

Tahadhari ya Kuwaokowa Wafuasi wanaoadhibiwa nchini China

Mkuu wa Chama cha Kikomunist cha Uchina, Jiang Zemin anashinikiza mashambulizi ya kitaifa dhidi ya Falun Gong kwa kuwarubuni**,** kuwakamata, kuwatesa na kuwauwa.

Imethibitishwa kuwa jumla ya wanafunzi 1061 wameteswa hadi kufa. Zaidi ya wanafunzi 100,000 wamekamatwa kinyume cha sheria na kupelekwa katika makambi ya kazi ngumu bila kushitakiwa. Zaidi ya wanafunzi 1,000 wenye akiri timamu wapelekwa katika hospitali za vichaa.

Mateso na mauaji ya wasio na hatia ya wafuasi wa Falun Gong yanabidi kutokomezwa. Wewe Unaweza Kusaidia !

Kwa msaada wasiliana na wafuatao:

- Vyombo na mashirika yanayojishughulisha na masuala ya haki za binadamu nchini.
- Mashirika ya Umoja wa Mataifa yaliyopo ndani na nje ya nchi.
- http//www.fofg.org kwa kutia sahihi katika orodha ya wanaopinga vitendo vya ukatili.